# Dart Jarida

Toleo la Mtandaoni.

Jarida la Mtandaoni | Toleo la 5 | Januari - Machi 2023




## DART yawakumbuka wazazi, siku ya Wanawake Duniani...

Katika kuadhimisha siku ya Wanawake duniani, watumishi wanawake wa Wakala Wa Mabasi Yaendayo Haraka(DART) wametoa msaada wa vifaa mbalimbali kwenye wodi ya wazazi katika Hospitali ya Mbagala Rangitatu jijini Dar es Salaam ....................*Uk1*

## RC Makalla atembelea miundombinu ya DART..........

Mkuu wa Mkoa wa Dar-es-Salaam Mhe Amos Makalla ameupongeza Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka-DART kwa usimamizi madhubuti wa mradi huo na kuridhishwa na kasi ya ujenzi wake ambapo amemtaka mkandarasi kuongeza kasi zaidi ............................ *Uk 2*



## Fursa za uwekezaji, kwenye miundombinu ya DART

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka - DART, unatoa fursa za uwekezaji kwa watu binafsi, makampuni, mashirika ya ndani na nje ya nchi na Taasisi za serikali kapitia maeneo yafuatayo;-

- Transit Oriented Development (TOD)
- Advertisement
  - Outdoor Advertising
  - Exclusive Station Naming Rights
- Business Centres
- Vending Machines.

*Nawasihi kila mmoja wetu kwa kutumia falsafa ya Kaizen kuendelea kuboresha huduma kwa kuzingatia misingi ya kibiashara na sheria zilizopo na zinazotuongoza ili tuweze kuweka historia iliyotukuka ya Wakala katika usafiri wa umma.*



# TAHARIRI

Wana Familia ya DART, nikiangalia mwaka uliopita, najivunia yale tuliyoweza kufanya kwa pamoja ambayo yameleta matokeo chanya tunapoendelea kutekeleza jukumu letu la kuendeleza usafiri nadhifu wa umma katika Jiji la kibiashara la Dar es Salaam, Tanzania. Kila mmoja wetu amejitahidi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuchangia katika matokeo tuliyopata hadi sasa, kwa kushirikiana na wadau wetu, wote kwa ujumla sekta binafsi na sekta ya umma, pamoja na watoa huduma wetu,wateja wetu,washauri wa masuala ya fedha, na washirika wa maendeleo.

Nimeguswa kwa jinsi mlivyojitoa na mnavyojituma, pamoja na juhudi za kila mmoja wetu hadi kuvuka lengo la ukusanyaji wa mapato (yatokanayo na nauli, na yasiyo ya nauli) viwango tulivyojiwekea kati ya mwezi na mwezi pamoja na changamoto zote zilizopo.

Hesabu tulizopata katika mwaka huu zinajieleza zenyewe. Nawapongeza kwa dhati kila mmoja wenu, katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita, tumeanzisha huduma mbalimbali za mtandaoni, ikiwemo huduma ya QR kodi katika GOT-AFCS, programu tumizi ya kununua tiketi kwa njia ya simu janja ijulikanayo Mwendokasi App), pamoja na huduma ya mtandao wa bure kwa umma (free WiFi).

Pia mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji nauli kwa kutumia kadi janja uko katika hatua za kukamilishwa na wataalamu wetu wa ndani wa Tehama na washauri wa kibiashara. Kwa kufanya hayo, tumeweza kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika kusimamia mapato ya nauli na yasiyotokana na nauli.

Hivyo, tuendelee hivyo hivyo na juhudi za makusudi kusimamia ukataji wa tiketi,usimamizi wa tiketi na usafiri waumma kwa ujumla. Pia, huduma mpya tulizoanzisha katika njia za Mloganzila na Kibaha, sanjari na huduma yetu mahsusi kwa wanafunzi ikisimamiwa na Uncle student, zinahitaji shukrani za pekee.

Katika kufanya haya yote,tunatekeleza lengo kuu la kuanzishwa Wakala wetu. Hii inamaanisha kuwa na mfumo wa kisasa wa usafiri wa umma wenye gharama nafuu kwa watumiaji lakini unaoleta faida kwa watoa huduma kwa kutumia mabasi yenye uwezo mkubwa na yanayokidhi viwango vya kimataifa, rafiki wa mazingira, kwa kutumia barabara maalum na kwa muda mfupi. Hivyo,tuendelee na ubunifu tulioonyesha.

Vilevile, tutafanya kila tuwezalo katika kipindi cha mwaka 2022/2023 kununua mabasi ya kisasa zaidi. Juhudi hizo zote zitawapatia wateja wetu huduma nafuu na kuwaaminisha kuwa DART ni Wakala wa Serikali unaomjali mteja.

Menejimenti ya DART na mimi binafsi, pamoja na kila mmoja wetu tuhakikishe tunaijenga DART yenye mafanikio zaidi, pia tutahakikisha ushirikiano wa hali ya juu kila wakati ili kuwezesha huduma bora ya usafiri wa umma kupitia BRT, pamoja na kuongeza na kusimamia ukusanyaji na udhibiti wa mapato.

Tunapouaga mwaka wa fedha wa 2021/2022, kwa niaba yangu binafsi na Menejimenti ya DART, nawashukuru sana kwa kujitoa kwenu kuhudumia jamii, tuendelee kufanya hivyo bila kuchoka katika kipindi cha 2022/2023.

Kwa hiyo, nawasihi kila mmoja wetu kwa kutumia falsafa ya Kaizen kuendelea kuboresha huduma kwa kuzingatia misingi ya kibiashara na sheria zilizopo na zinazotuongoza ili tuweze kuweka historia iliyotukuka ya Wakala katika usafiri wa umma.

Naendelea kuwategemea, na nina furaha kuendelea kufanya kazi nanyi katika mwaka wa fedha wa 2022/2023.

***Nawatakia watumishi wenzangu wote na wanafamilia ya DART kwa ujumla heri ya mwaka mpya na wenye furaha wa fedha 2022/2023. (nawategemea sana kufanya kazi kwa bidii) tuweze kufanikisha lengo la***


**BODI YA WAHARIRI**

**Dkt. Edwin Mhede**
*Mwenyekiti*

**WAJUMBE**

Dkt. Eliphas Mollel
William Gatambi
Elias Malima
Martha Komba
Shaban Kajiru
Christian Luoga
Ange Hida
Paxley Mwenitete
Kennorton Luhindi
Ayubu Sanga

*Jarida limendaliwa na*
**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka**
**Ubungo Maji, Barabara ya Morogoro**
**S.L.P 724, 16103 Dar es Salaam**

# DART yawakumbuka Wazazi Siku ya Wanawake Duniani.




Katika kuadhimisha siku ya Wanawake duniani, watumishi wanawake wa Wakala Wa Mabasi Yaendayo Haraka - DART wametoa msaada wa vifaa mbalimbali kwenye wodi ya wazazi katika Hospitali ya Mbagala Rangitatu ya Jijini Dar-es-Salaam.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi misaada hiyo yenye thamani ya shilingi Milioni nane, Mwenyekiti wa wanawake DART Bi Mwamvua Stambuli amesema wanatambua mchango wa kinamama ndio maana wameamua kutoa mchango huo kwa kuwa hospitali hiyo ipo karibu na miundombinu ya BRT awamu ya pili ambayo iko katika hatua mbali mbali za kukamilishwa.

“Tunajivunia kuongozwa na Rais Mwanamke Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan, hivyo sisi kama wakinamama wenzake tunamuunga mkono kwa kuendelea kusaidia wakinamama wenzetu ili lengo lake la kuwaletea maendeleo watanzania litimie” Alisema.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo Dkt Ally amepongeza na amewashukuru wanawake na uongozi mzima wa DART kwa moyo wa ukarimu na upendo waliouonyesha kwa kuona umuhimu wa kuwakumbuka wagonjwa hasa wazazi.

Alisema hospitali hiyo iliyo kwenye Manispaa ya Temeke inahudumia wagonjwa toka sehemu mbalimbali za Wilaya hipo Pamoja na Mikoa ya Jirani ambapo kwa siku inahudumia wagonjwa wapatao 1000 hadi 1200, wakimwemo wakina mama wanaofika kujifungua ambao idadi yao ni 30 hadi 40.

Dkt. Mussa alisema kutokana na Hospitali hiyo kuhudumia idadi kubwa ya wagonjwa, kumekuwepo wa uhitaji wa misaada mingine Zaidi ili waweze kuwasaidia wagonjwa hasa wale wanaotoka katika familia masikini nza zile za pembezoni, hivyo akawaomba wadau mbali mbali kujitokeza kama walivyofanya kinamama wa DART ili kuwashika mkono.

> *“Tunajivunia kuongozwa na Rais Mwanamke Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, hivyo sisi kama wakinamama wenzake tunamuunga mkono kwa kuendelea kusaidia wakinamama wenzetu ili lengo lake la kuwaletea maendeleo watanzania litimie”*

# RC Makala atembelea Miundombinu ya DART, Aridhishwa na Kasi ya Ujenzi

Mkuu wa Mkoa wa Dar-es-Salaam Mhe Amos Makalla ameupongeza Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka-DART kwa usimamizi madhubuti wa mradi huo na kuridhishwa na kasi ya ujenzi wake ambapo amemtaka mkandarasi kuongeza kasi Zaidi ili umalizike kwa wakati.




Akizungumza hivi karibuni Jijini Dar es Salaam wakati akikagua tuta linalotenganisha barabara za Mandela na Kilwa na baadaye kwenye barabara za Kilwa na Sokoine, RC Makala alisema ni vyema DART ikaongeza usimamizi ili barabara hizo ziweze kukamilika kwa muda waliojiwekea katika mkataba.

"Nawapongea kwa hatua mlizofikia, lakini pia kwa namna mnavyojitahidi kufungua njia mbali mbali katika mkoa wa Dar es Salaam na nyingine ambazo zinafika hadi mkoa wa Jirani wa Pwani" Alisema.

Katika ziara hiyo Mkuu huyo wa Mkoa aliipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mh. Rais Dr. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake katika kuleta maendeleo kwenye sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwemo ya usafiri wa umma hususan katika BRT na SGR Pamoja na bandari ya Dar es Salaam miradi ambayo pia aliitembelea. Alisema kukamilika kwa miundombinu ya DART katika awamu zote sita kutachochea ukuaji wa uchumi sio kwa Dar es Salaam pekee bali kwa nchi nzima kwani msongamano wa magari unawapotezea wananchi muda mwingi ambao wangeutumia katika shughuli za uzalishaji.



Katika hatua nyingine, Mkuu wa Mkoa alimpongeza Mkandarasi anayeendelea na ujenzi wa BRT awamu ya Pili kuelekea Mbagala Rangitatu Kampuni ya Sino Hydro kwa kazi inayoendelea kufanyika licha ya changamoto mbalimbali zinazojitokeza ikiwemo ya watu kulipwa fidia na kugoma kuhama.

Aidha mkuu huyo wa Mkoa alisisitiza wadau wote wa mradi wa BRT kutoa ushirikiano wakati wote ujenzi unapoendelea, kwa kutoa huduma muhimu na kwa wakati pale zinapohitajika, mfano maji,umeme na usalama, jambo litakalosaidia ujenzi kukamilika kwa wakati.

RC Makalla pia aliwaonya wafanyabiashara ndogo ndogo na vyombo wa usafiri kuacha mara moja kukatiza ama kufanya shughuli zao katika miundombinu inayoendelea kujengwa ya BRT, ambapo alimuagiza Katibu Tawala na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kuwahamisha wafanyabiashara wote waliovamia miundombinu ya ujenzi wa mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka.

# DART Yashiriki Kikao cha Tatu Serikali Mtandao.





Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) umeshiriki katika kikao cha tatu cha Serikali Mtandao kilichofanyika hivikaribuni katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa (AICC) Jijini Arusha.

Katika kikao hicho ambacho Menejimenti ya Wakala uliwakilishwa na Mkurugenzi wa Utawala Rasilimaliwatu na Mawasiliano Dkt. Eliphas Mollel, lengo kuu ilikuwa kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhimiza matumizi ya TEHAMA katika kuboresha utendaji kazi wa Taasisi za Umma.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao hicho kilichoratibiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao, Waziri wa Nchi,Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Jenista Mhagama alisema TEHAMA ni nyenzo muhimu na wezeshi katika kufikia Mapinduzi ya nne ya viwanda. “Katika zama hizi huwezi kuendelea bila kuwa mbobezi katika matumizi sahihi ya TEHAMA, ndiomaana Serikali ya Awamu ya Sita inasisitiza matumizi ya Teknolojia hiyo katika kuwaletea watanzania maendeleo lakini pia kurahisisha Maisha na utendaji kazi wa serikali” Alisema.

Aidha Waziri Jenista, ameishukuru ***Mamlaka ya Serikali Mtandao - eGa*** Pamoja na wadau wa teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

Mkutano huo uliofanyika kwa siku tatu Jijini Arusha ulibeba kaulimbiu ya “Mifumo jumuishi ya TEHAMA




kwa utoaji bora wa huduma za Umma” uliwakutanisha wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao kujadiliana juu ya mafanikio, changamoto pamoja na kuweka mikakati ya kukuza Serikali Mtandao nchini.

Utekelezaji wa jitihada za serikali Mtandao ni moja ya maeneo muhimu ya maboresho yaliyofanyika katika utumishi wa Umma, ambayo yamesaidia kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma bora kwa Umma na kufanya zipatikane kwa urahisi,haraka na kwa gharama nafuu.

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka umekuwa mdau muhimu wa masuala ya TEHAMA ambapo umesimika na unatumia mifumo mbali mbali katika kurahisisha utendaji kama vile mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa nauli AFCS, Pamoja na mifumo mingine ambayo inaadaliwa ikiwemo ule wa kuomgoza na kuangalia mwenendo wa Mabasi.

# Kongamano la Nishati salama DART kuwa kinara kitaifa katika kupunguza hewa ukaa kufikia 2030.



Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) imejizatiti kupunguza hewa ukaa na hivyo kuwa kinara katika malengo ya Tanzania iliyojiwekea ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi kwa kuondosha hewa ukaa kwa asilimia 30 hadi 35 kufikia mwaka 2030.

Hayo yamebainishwa na Mtendaji Mkuu wa DART Dr. Edwin P. Mhede wakati akifungua kongamano la nishati salama katika usafirishaji ambalo limefanyika kwa mara ya kwanza Dar es salaam Tanzania Machi 20, 2023.

Dr. Mhede alisema mwaka 2014 Tanzania ilikuwa inazalisha hewa ukaa kwa asilimia 57.6 kiasi ambacho kilianza kupungua baada ya DART kuanza kutoa huduma ya usafiri Dar es salaam mwaka 2016 iliyopelekea kuondoshwa kwa daladala takribani 900 zilizochangia kwa kiasi kikubwa katika uchafuzi wa hewa.

"Mabasi ya DART yanatumia injini za kisasa zinazotumia Mafuta ya Euro IV ambayo yamekubalika kidunia kwa kutoa hewa ukaa kidogo ikilinganisha na injini za daladala. Malengo yetu ni kuelekea kwenye Injini za Euro VI, Gesi asilia hadi mabasi ya umeme ambayo hayatoi kabisa hewa ukaa" alisema Dr. Mhede.

Katika kuunga mkono juhudi za Mradi wa Solutions Plus yenye malengo ya kuondosha kabisa hewa ukaa, Dr. Mhede alisema Wakala wa DART ina mpango wa kujenga miundombinu ya kuchajia vyombo vya moto vinavyotumia umeme katika Kituo Kikuu cha Kimara na Morocco vitakavyotumiwa na vyombo vya usafiri vya umma na binafsi.

Kongamano la Afrika kuhusu nishati salama katika usafirishaji linafanyika kwa siku tano kwa kuwakutanisha wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi ili kujadili namna bora ya kuelekea kwenye matumizi ya nishati ya umeme ambayo ni salama kwa mazingira.






# Madereva BRT wafundwa.



Wakala Wa Mabasi Yaendayo Haraka DART, umeendesha mafunzo kwa madereva wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Karakana ya Jangwani kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kukabiliana na ajali za barabarani, Pamoja na majanga yanayoweza kujitokeza wakati wanatekeleza majukumu yao ya kila siku.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo, kaimu Meneja wa Mipango na usafirishaji DART Mhandisi. Mohammed Kuganda alisema lengo kuu la mafunzo hayo ni kuwakumbusha wajibu wao katika kutoa huduma bora kwa wananchi, lakini pia kujua dira na mwelekeo waw akala ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi Zaidi.

Alisema suala la elimu na kuongeza maarifa ni la kila siku hivyo Wakala licha ya kutoa mafunzo na kukutana nao mara kwa mara utaendelea kutafuta fursa mbali mbali za kuwajengea uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi.

Mhandisi Kuganda aliongeza kuwa, lengo lingine la mafunzo hayo ni kuainisha changamoto zinazowakabili madereva katika mfumo wa BRT ili kwa Pamoja waje na majibu ya namna bora ya kuzitatua ili Kwenda sambamba na Dira, Malengo, Dhiman na mwelekeo wa DART katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Aidha, msisitizo uliwekwa katika matumizi ya lugha zenye staha na rafiki kwa makundi yote kwakuwa usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka unahudumia makundi mengi tofautitofauti katika Jamii.

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka umekuwa ukiendesha mafunzo na semina za mara kwa mara kwa wadau na watendaji wake ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja kwani huduma hiyo inagusa Maisha ya watanzania Zaidi ya laki mbili na nusu wanaotumia Mabasi hayo kwa usafiri wa kila siku.

*Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka umekuwa ukiendesha mafunzo na semina za mara kwa mara kwa wadau na watendaji wake ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja kwani huduma hiyo inagusa Maisha ya watanzania Zaidi ya laki mbili na nusu wanaotumia Mabasi hayo kwa usafiri wa kila siku.*



# Mradi wa DART waendelea kuwa Kioo cha usafiri wa Umma Afrika Mashariki

WAKALA wa Mabasi yaendayo Haraka (DART) umeendelea kuwa kielelezo cha mfano kwa nchi za Afrika Mashariki katika kusimamia na kuendesha huduma ya usafiri wa uuma jambo linalofanya wadau mbalimbali kutoka nchi za Afrika kuvutiwa kuutembelea kwa ajili ya kujifunza.

Akizungumza hivi karibuni Jijini Dar es Salaam wakati wa ziara ya wadau wa usafiri wa umma kutembelea miundombinu ya DART, Kaimu Meneja wa Mipango na Usafirishaji wa Wakala huo Mhandisi Mohamed Kuganda alisema upekee wa mradi huo katika eneo zima la Afrika Mashariki unafanya wageni wengi kuvutiwa kujifunza namna unavyoendeshwa.



“Tumekuwa tukipokea wageni mbali mbali kutoka sehemu nyingi Afrika ambao lengo lao kuu ni kujifunza jinsi tunavyoendesha mradi wetu, kama mnavyoona leo tuko na wageni kutoka nchini Kenya ambao ni wadau wa usafiri wa umma kutoka taasissi za usafirishaji na miradi ya Maendeleo (ITDP) na Wakala wa Barabara nchini Kenya KENHA, wamekuja kujifunza kwa lengo la Kwenda kuanzisha mradi kama huu nchini kwao” Alisema.

Amesema upekee wa mradi huo na namna unavyoendeshwa kwa ubia baina ya Serikali na sekta binafsi kunachangia kunawavutia wadau wa sekta ya usafiri wa umma kutoka katika mataifa mbalimbali kuja kujionea na kujifunza namna Tanzania ilivyoweza kusimamia mradi huo.

Aidha Mhandisi Kuganda amesema matumizi ya teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kukata tiketi za safari katika mradi wa DART imekuwa pia sababu na kivutio kikubwa cha wageni mbali mbali kutoka nje ya Tanzania kutembelea mradi huo.

Kwa upande wake kiongozi wa msafara huo ambaye ni Mkurugenzi wa Usanifu wa Usalama wa Barabara na Mazingira wa Wakala wa barabara nchini humo KENHA Mhandisi.Ezekiel Wafula, amesema mfumo wa usafiri wa umma nchini Tanzania ni wa pekee na wakuigwa kwa mataifa mengine ambayo tatizo la msongamano wa magari katika miji mikubwa limeendelea kuwasumbua.

“Tumejionea wenyewe namna mradi huu unavyofanya kazi, zamani ilikuwa sio rahisi kwa nchi za kiafrika Kwenda kujifunza katika nchi nyingine za kiafrika ilizoeleka kila kitu lazima tukajifunze katika mataifa ya ulaya na kwingineko ila kwa Tanzania hii ni hatua kubwa sana mliyopiga” Alisema Mhandisi. Wafula.

Alisema kuwepo kwa mradi kama wa DART kunachangia kupunguza hewa ya ukaa inayosababishwa na ongezeko la magari mijini kwani mabasi machache yatatumika na magari mengi ya binafsi yatapungua barabarani hivyo kuhifadhi mazingira.

Naye Katibu wa Kaunti ya Mombasa Bw.Jeizan Faruk alisema katika mji wao pia wanatarajia kuanzisha mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka kwa lengo la kutatua changamoto ya usafiri wa umma katika mji huo wa Pwani ya Kenya.



# Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu yaupongeza Wakala wa DART



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu yaupongeza Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) kwa kuandaa mpango unaotoa fursa ya kufanya biashara kwa wafanyabiashara wadogo wadogo katika Kituo Kikuu cha Mabasi Yaendayo Haraka Mbagala Rangitatu.

Pongezi hizo zimetolewa Machi 18, 2023 na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili katika barabara ya Kilwa kuelekea Mbagala Rangitatu.

Aidha Mheshimwa Kakoso alitoa pongezi hizo baada ya Kamati yake kuhoji endapo kunampango ulioandaliwa kwa ajili ya Wafanyabiashara wadogo wadogo pindi huduma itakapoanza kutolewa na ndipo alipothibitishiwa hilo na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Usafirishaji wa DART Mhandisi Fanuel Kalugendo.


Katika ziara hiyo kamati hiyo iliweza kupokea taarifa kuhusu Ujenzi wa Miundombinu ya DART ikiwa ni pamoja na majina na urefu barabara pia hatua zilizofikiwa mpaka sasa.

Aidha Kamati hiyo ilipata nafasi ya kutembelea Awamu ya Pili ya Mradi ambayo iko katika hatua za mwisho na huduma za usafiri zinatarajiwa kuanza hivi karibuni ambapo ziara hiyo ilihitimishwa jkatika katika kituo Kikuu cha Mabasi hayo kilichopo eneo la Mbagala Rangitatu

Mradi wa DART unatekelezwa katika Awamu Sita, ambapo Awamu ya Kwanza ya Mradi ieshakamilika na huduma inatolewa kuanzia Kimara hadi Kivukoni na tawi la kutoka eneo la Fire hadi Gerezani Kariakoo na Tawi la kutoka Magomeni hadi Morocco. Awamu ya Pili ya Mradi katika barabara ya Kilwa ujenzi wake unaendelea kama ilivyo katika Awamu ya Tatu katika barabara ya Nyerere kuelekea Gongolamboto.

# Ifahamu Kaizen

KAIZEN ni uboreshaji endelevu, na 5S (Sasambua, Seti, Safi sha, Sanifisha na Shikilia) ni moja ya njia za utekelezaji wake. 5S ni muhimu katika kutengeneza eneo la kazi lililo salama, lenye starehe na lenye ufanisi.



# Ziara ya Naibu Waziri TAMISEMI







# Intern wapya Wakipokelewa







# Tukiwa Gemba








# Uncle Student








DART
DAR RAPID TRANSIT AGENCY
Dar City Navigator sasa ni
Mwendokasi App
Home
Transaction history
Incident Reporting
Service disruption
Information
Contact us
Settings
Facebook
Instagram
Twitter
Mwendokasi
Where to ?
Add
Home
Tap to set home address
Work
Tap to set work address
Advertise with us
Get Ticket
Tickets
Pakua Sasa
Available on the Google Play
Pakua Sasa
Download on the App Store
DARTMwendokasi
DART TV
0800 110 147
www.dart.go.tz